# HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA

# TANGAZO

**02/12/2024**

## FURSA ZA UWEKEZAJI KWA MFUMO YA UBIA (PPP)

Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela kupitia Baraza la Madiwani lililoketi tarehe 05/11/2024 inawatangazia na kuwajulisha Wananchi, Taasisi, Mashirika, Kampuni, Wafanyabiashara na wadau wote wa Maendeleo ndani na nje ya Manispaa ya Ilemela kuwa, Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela ina maeneo mazuri yanayohitaji uwekezaji wa aina mbalimbali kwa utaratibu wa Ubia (PPP).

Mpango huu wa uwekezaji utatekelezwa kwa kuzingatia sera ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP). Sheria ya 'PPP' ya mwaka 2010 Sura 103 na Kanuni za 'PPP' za mwaka 2020 pamoja na marekebisho yake imeweka utaratibu wa kuongeza ubora na ufanisi wa huduma Pamoja na kupanua wigo wa vyanzo mbadala vya bajeti ya Serikali ili kugharamia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa kushirikisha Sekta Binafsi.

Maeneo yanayotangazwa kwa utaratibu huu ni**: -**

| Na | Eneo/Mahali | Ukubwa | Wazo biashara/pendekezo |
|---|---|---|---|
| 1. | **Eneo la uwekezaji Kirumba** | **5,942M$^2$** | Eneo hili linafaa kwa kujenga nyumba za kupangisha 'Apartments za ghorofa' na zipo nyumba chache za Halmashauri n.k |
| 2. | **Eneo la Soko la Nyasaka** | **31,020M$^2$** | Eneo hili linafaa kwa:-<br>- Kumbi za kisasa (Convention Centre and Multipurpose Conference halls)<br>- Kujenga nyumba za kupangisha (Apartments)<br>- Sehemu ya mapumziko na burudani (recreational and entertainment centre) |

| Na | Eneo/Mahali | Ukubwa | Wazo biashara/pendekezo |
|---|---|---|---|
| 3. | **Eneo la Soko la zamani Nyamanoro Kata ya Ibungilo:** | **6,425M2** | Eneo hili lipo pembezoni mwa Barabara Kuu iendayo *'Airport'* mkabala na njia iendayo Kanisa Kuu la RC, lipo ukanda wa hoteli na linafaa kwa kujenga Hotel na nyumba za kupangisha (Apartments) n.k |
| 4. | **Eneo la stendi ya zamani Buzuruga na soko** | **20,445$M^2$** | Eneo hili kwa sasa linatumika kama kituo cha kupakia na kushusha abiria hususani daladala sambamba na biashara za maduka. Eneo hili linapendekezwa kujenga kitega Uchumi pasipokuathiri shughuli za usafirishaji wa abiria wa daladala |
| 5. | **Eneo la stendi ya daladala Buswelu** | **19,300$M^2$** | Eneo hili limetengwa kwa ajili ya stendi ya daladala, pia linafaa kujenga kumbi na hotel. Eneo hili lipo pembezoni mwa Barabara Kuu na linapakana na Soko Kuu la Buswelu liitwalo Kabwalo kwa upande wa chini. |
| 6. | **Maeneo ya Buffer zone Nyamhongolo na maeneo mengine** | **Ukubwa utategemea hitaji la mwekezaji** | Maeneo yote ya 'buffer' yanafaa kwa biashara mbalimbali kama vile 'Car wash', Michezo ya Watoto, show rooms, bustani gardeni' n.k |

Maeneo yote haya yapo katika maeneo ya makazi Katikati ya mji yanafikika sambamba na uwepo wa huduma zote za msingi yaani Umeme, Maji, Usafiri na kuwa karibu na taasisi nyingine za msingi kama Hospitali, Soko n.k

Aidha, Tunakaribisha Mawazo zaidi ya Uwekezaji na Biashara ambayo Halmashauri itashirikiana na Sekta binafsi, Mashirika na Taasisi mbalimbali. Pia wadau wote wa Maendeleo mnakaribishwa kutembelea maeneo haya na mengine mengi ili kuja na Mawazo zaidi ya uwekezaji na Biashara.

**MASUALA YA KUZINGAITA**

i. Utaratibu huu wa Ubia (PPP) ni makubaliano ya Ubia baina ya Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela na Mbia kutoka sekta Binafsi, Taasisi, Shirika au Kampuni ambaye atatekeleza jukumu la Halmashauri kwa niaba ya Halmashauri kwa muda Maalumu.
ii. Mbia atawekeza fedha, ufundi na uendeshaji na atapokea malipo kutoka kwa watumiaji wa huduma, Serikali au njia zote mbili kutokana na utekelezaji wa jukumu husika.
iii. Uwezo wa serikali na watumiaji wa huduma kumudu gharama za mradi na gharama za huduma katika kipindi chote cha uendeshaji.
iv. Mradi utazingatia thamani ya fedha ikilinganishwa na utekelezaji wa Mradi kwa ununuzi wa kawaida unaotumia bajeti ya serikali.
***v.*** Kwa yeyote mwenye uhitaji wa kuwekeza kwa utaratibu huu, awasilishe **barua ya kusudio/nia (Expression of interest)** ikiambatanishwa na **Wazo Mradi (Concept note) kwa kuzingatia muundo (format) ulioambatanishwa.** ***Wasilisha maombi kabla au ifikapo tarehe 31.12.2024***

Kwa mawasiliano zaidi, fika ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilemela au wasilisha kupitia anuani ifuatayo: -

*MKURUGENZI WA MANISPAA,*
*HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA,*
*S.L.P. 735,*
***ILEMELA – MWANZA***
***Email:*** *md@ilemelamc.go.tz*

*Tangazo hili limetolewa na;*

Ummy M. Wayayu
**MKURUGENZI WA MANISPAA**
**ILEMELA**

MKURUGENZI HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA S.L.P. 735 MWANZA

# CONCEPT NOTE DEVELOPMENT GUIDE

## *FOR POTENTIAL*

## PUBLIC - PRIVATE PARTNERSHIP INITIATIVES

### Executive summary of the report

### Project description

**Statement of the problem**

**Project objectives and outputs**

**Geographic description of the project**

**Needs and options analysis**

**Suitability for PPP**

- Project administration
- Relevance of the project to the National Development Priorities;
- Economic feasibility
- Project financing analysis, including project costs, revenues and cash flow;
- Marketing and commercial assessment
- Value for money analysis
- Affordability assessment
- Assessment of risk
- Stakeholder's analysis
- Legal requirement
- Implementation Action plan
- Any other information relevant to the project
- Include annexes, if any